MAJI TANZANIA
TOLEO NA 019
JANUARI- MACHI, 2023

# Huduma ya majisafi inatolewa kwa weledi

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema mkakati wa kufikisha huduma ya majisafi katika makazi ya wananchi unafanyika kwa weledi kwa kuzingatia maelekezo ya viongozi wakuu wa nchi.

Mhe. Majaliwa amesema hayo leo tarehe 16 Machi 2023 wakati akifungua rasmi Wiki ya Maji na kuzindua mradi wa majisafi wa Tegeta jijini Dar es salaam. Moja ya maeneo yanayohudumiwa na mradi huo wakazi wake hawajawahi kupata huduma ya majisafi ya bomba katika makazi yao.






# Bil. 24.4 kufanikisha huduma ya majisafi Tinde - Shelui




## Aweso ahutubia UN kuhusu maji



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amehutubia Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Marekani.

Mhe. Aweso amemwakilisha Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo.

# Bil. 24.4 kufanikisha huduma ya majisafi Tinde - Shelui






Moja ya tanki la kuhifadhi maji katika mradi huo.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Philip Isdor Mpango ameweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwa mji wa Tinde. Hafla ya hiyo imefanyika 2023 katika eneo la tanki la maji la Buchama nje kidogo ya mji wa Tinde mkoani Shinyanga.

Mradi unagharimu Tshs shilingi bilioni 24.4, na unatarajia kuhudumia wakazi wa miji ya Tinde na Shelui.

Mhe. Dkt.Mpango amesema dhamira ya serikali ya awamu ya sita ni kuhakikisha inatekeleza miradi ambayo itawezesha huduma endelevu ya majisafi na hivyo kusaidia kukuza uchumi wa Taifa.

Amewataka wadau wa sekta ya maji kuongeza weledi katika usimamizi wa miradi ya maji pamoja na utunzaji wa rasilimali za maji ili kuwezesha lengo la serikali la kuifanya miradi hiyo iwe endelevu.

Kwa upande wake Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Wizara itaendelea kufuatilia na kusimamia kwa makini utekelezaji wa miradi ya maji ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kutoa huduma kwa wananchi.




Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango akiweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Tinde-Shelui wenye thamani ya Tshs Bilioni 24.4

# Huduma ya majisafi inatolewa kwa weledi

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema mkakati wa kufikisha huduma ya majisafi katika makazi ya wananchi unafanyika kwa weledi kwa kuzingatia maelekezo ya viongozi wakuu wa nchi.

Mhe. Majaliwa amesema hayo leo tarehe 16 Machi 2023 wakati akifungua rasmi Wiki ya Maji na kuzindua mradi wa majisafi wa Tegeta jijini Dar es salaam. Moja ya maeneo yanayohudumiwa na mradi huo wakazi wake hawajawahi kupata huduma ya majisafi ya bomba katika makazi yao.

Amesema kila kiumbe hai na mazingira vyote vinahitaji maji na wananchi wanapopata huduma ya majisafi, ni maendeleo makubwa katika nchi na kwa mtu binafsi.

"Upatikanaji wa majisafi ni agenda ya kudumu,na inafanyika hatua kwa hatua ili wananchi wapate majisafi ya uhakika kwa asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025 kamaSerikali ilivyopanga" Mhe.Majaliwa amesema na kusisitiza kuwa kazi ya kusambaza maji ni kazi endelevu na kila mwananchi atafikiwa hadi maeneo ya pembezoni.

Amesema Serikali imeanza kutumia vyanzo vikubwa vya maji ili kusambaza maji kwa wananchi, ikiwemo maziwa makuu. Pia, katika kukabilina na mabadiliko ya tabia nchi amesema miradi ya kimkakati inatekelezwa ikiwamo ujenzi wa bwawa la Farkwa na Kidunda, na kuimarisha huduma ya maji katika jiji la Dodoma kwa kutumia bwawa la Mtera.

Mhe. Majaliwa amesema Serikali inao uwezo wa kifedha ambapo vijiji 9,144 vinapata huduma ya maji na lengo ni kufikia vijiji 12,319 na amewataka wananchi kutunza vyanzo vya maji ili huduma ya maji katika makazi yao iwe endelevu na kuitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) kuhakikisha maeneo yote yanayotoa huduma kwa umma yanapata majisafi.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea awali, amesema Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hataki kusikia wananchi wakipata adha ya huduma ya maji na kusisitiza maunganisho ya maji yafanyike ndani ya siku saba za kazi baada ya kupokea maombi.

Mhe. Aweso amefafanua kuwa ni haki ya mwananchi kupata huduma ya maji, ila mwananchi anao wajibu wa kulipia huduma hiyo kadri anavyoitumia.

"Miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita utekelezaji wa bajeti ya Sekta ya Maji umepanda kutoka asilimia 50 hadi asilimia90" Mhe. Aweso amesema na kusisitiza Tanzania inayo maji ya kutosha na watendaji wa Sekta ya Maji wamejipanga kutekeleza miradi ya maji kwa sababu fedha za kazi hiyo zipo.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akizindua mradi wa maji wa Tegeta, na Wiki ya Maji 2023. Mradi utanufaisha zaidi ya wakazi laki nne.



Mradi wa maji wa Tegeta utanufaisha zaidi ya wakazi zaidi ya laki nne na nusu na umehusisha mfumo wa usambazaji maji kati ya Makongo na mji wa Bagamoyo,wakati kazi inaendelea tayari wakazi elfu 37 wameshapata huduma.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa katika mdahalo wa siku 365 uliogusa Sekta ya Maji, ambapo amesisitiza fedha za kutekeleza miradi ya maji zipo, na kazi zinafanyika kufikisha maji kwa umma. Tukio hilo limefanyika jijini Dar es salaam



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja akieleza masuala ya kitaalamu katika mdahalo wa siku 365 uliogusa Sekta ya Maji, jijini Dar es salaam






Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhandisi Nadhifa Kemikimba kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, hafla imefanyika Ikulu ya Chamwino Dodoma.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhandisi Cyprian Luhemeja kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, hafla imefanyika Ikulu ya Chamwino Dodoma.



# Vijiji 56 Ruangwa na Nachingwea kupata Majisafi



Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imesaini mradi mkubwa wa maji wa Nyangao - Ruangwa - Nachingwea utakaowezesha kufikia lengo la kitaifa la upatikanaji wa huduma ya majisafi vijijini kwa zaidi ya asilimia 85.

Mradi huu, unajumuisha vijiji 34 vya Wilaya ya Ruangwa, vijiji 21 vya Wilaya ya Nachingwea na Kijiji kimoja katika Wilaya ya Lindi vyenye wakazi wanaokadiriwa 128,657.

Chanzo cha mradi uliosainiwa ni Mito Nyangao na Chiue iliyopo Wilaya ya Lindi. Kwa pamoja chanzo kitakuwa na uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita 15,000,000 kwa siku, wakati mahitaji ya maji kwa vijiji vyote vilivyopangwa kuhudumiwa na mradi kwa miaka 20 ijayo ni wastani wa lita 6,912,000 kwa siku.

Ili mradi ukamilike kwa wakati, mradi huu umegawanywa katika sehemu (Lots) mbili, ambapo kila sehemu itakuwa na mkandarasi wake.

Sehemu ya kwanza itahusisha ujenzi wa dakio la maji, ujenzi wa bomba kuu la maji mtiririko (gravity main) na maji ya msukumo (pumping main) jumla ya km 85 yenye ukubwa wa kipenyo cha mm 500. Sehemu hii itatekelezwa na Kampuni ya STC Construction Company Limited ya Dar Es Salaam kwa gharama ya Sh. 12,417,026,276.92 bila Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa muda wa miezi kumi na nne (14).

Sehemu ya pili inayohusisha kazi zote zilizobaki, itatekelezwa na Mkandarasi Emirate Builders Co. Limited ya Dar Es Salaam kwa Sh. 107,138,897,161.00 bila Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa muda wa miezi ishirini na sita (26). Kampuni zote mbili ni za Tanzania.




Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi akiongea na wananchi wakati wa hafla ya kusaini mradi wa maji wa Nyangao - Ruangwa – Nachingwea




Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement Kivegelo akieleza kuhusu mradi wa Nyangao - Ruangwa - Nachingwea

# Aweso ahutubia UN kuhusu maji

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amehutubia Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Marekani.

Mhe. Aweso amemwakilisha Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo.

Hotuba hiyo imehusu umuhimu wa maji katika mahitaji mbalimbali ya maisha, pamoja na uwekezaji katika Sekta ya Maji.

Katika mkutano, Tanzania imebeba agenda mbili ambazo ni utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Tatu (Water Sector Development Programe III) ambayo inahitaji Dola za Marekani bilioni 6.47 kwa kipindi cha 2022-2025.

Pia, Uwekezaji katika Sekta ya Maji ili kufikia Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (Tanzania Water Investment Programme 2023-2030). Programu ambayo bado inaandaliwa na ipo hatua za mwisho kuzinduliwa ikikadiriwa kuwa na bajeti ya zaidi ya Dola za Marekanii bilioni 25 na itazinduliwa Mei 2023.







Viongozi wa Wizara wa Maji wakiwasili ofisi za Wizara mara baada ya kuapishwa. Kushoto ni Katibu Mkuu Mhandishi Nadhifa Kemikimba, Waziri Mhe. Jumaa Aweso, Naibu Katibu Mkuu Mhandishi Cyprian Luhemeja na Naibu Waziri Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi



# Mradi wa Maji wa Miji 28 kuimarisha huduma ya maji Songea




Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba (kushoto) akisaini mkataba wa ujenzi wa Mradi wa maji wa miji 28, Songea.

Wizara ya Maji imesaini mkataba na Mkandarasi kampuni ya China Civil Engineeering Construction Corporation (CCECC) ili kujenga mradi wa maji wa Miji 28 katika Mji wa Songea wenye thamani ya Tshs bilioni 145.7.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akimwakilisha Waziri wa Maji amesema mradi huo ukikamilika utakua na uwezo wa kuzalisha maji kutoka lita milioni 11.58 kwa siku hadi kufikia lita milioni 42.581 kwa siku.

Amesema mradi huo utamaliza kero ya maji katika Manispaa ya Songea kwa sababu upatikanaji wa maji utakua wa uhakika na utakuwa na uwezo wa kuwahudumia wananchi zaidi ya laki nne.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba akizungumza kabla ya kusaini mkataba huo amesema mradi huo utakapokamilika utakuwa na uwezo kuhudumia wananchi wa Songea hadi mwaka 2045, ambapo idadi ya wakazi wa Songea inatarajiwa kuwa zaidi ya 400,000.

Amezitaja kazi ambazo zitafanyika kwenye mradi huo kuwa ni ujenzi wa bwawa lenye uwezo wa kujaza maji lita milioni 4.8, ujenzi wa mtambo wa kuchuja maji lita milioni 16 kwa siku, ujenzi wa matanki 10 yatakayosafirisha maji kutoka kwenye bwawa hadi kwenye matenki pia usambazaji wa maji wenye kilometa zaidi ya laki nne.



Mkataba ukionyeshwa kwa wananchi waliohudhuria hafla hiyo baada ya kusainiwa na Serikali,Songea.

Hafla hiyo ilihushuhudiwa na maelfu ya wananchi pamoja na viongozi mbalimbali wa mkoa.

# Wizara ya Maji Kimataifa


Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga pamoja na ujumbe wa Wizara ya Maji wameshiriki Mkutano maalum unaohusiana na Masuala ya Huduma ya Maji Duniani World Water-Tech Innovation Summit (WWIS) 2023 jijini London.

Mkutano huo unaratibiwa na serikali ya Uingereza.

Akizungumza katika mkutano Waziri Aweso ametoa wito kwa wadau wa sekta ya Maji duniani kuongeza jitihada katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwani ndio changamoto inayokabili dunia kwa sasa.

Naye, Katibu Mkuu Mhandisi Sanga akishiriki katika mjadala wa wataalamu alisisitiza kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na kuwekeza katika uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa ili kuhakikisha yanakua sehemu ya kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mkutano huo umejadili namna bora ya kuboresha mifumo ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira ili kuendana na ongezeko la watu katika maeneo ya mijini.




Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongoza ujumbe wa Wizara ya Maji katika mkutano maalumu unaohusiana na Masuala ya Huduma ya Maji Duniani World Water-Tech Innovation Summit (WWIS) 2023 jijini London. Hivi sasa Mhandisi Anthony Sanga Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

# RUWASA Yazidi kuimarishwa kwa vifaa, Aweso awakabidhi magari mapya 10

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amemkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mhandisi Clement Kivegalo magari 10 mapya yaliyogharimu Sh bilioni 1.5. ili yatumike katika shughuli za Wakala huo sehemu mbalimbali mikoani.

Hafla ya makabidhiano ya magari hayo imefanyika jijini Dodoma.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi magari hayo Mhe. Aweso amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa nia yake ya dhati ya kuhakikisha changamoto za watumishi katika Wizara ya Maji zinapatiwa ufumbuzi.

Pia amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa wakala huo kuhakikisha magari hayo yanatumika kufanikisha ufuatiliaji wa miradi na sio kinyume na hapo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo amesema uhitaji wa magari kwa ajili ya Wakala huo ni magari 398 nchi nzima na magari yaliyopo ni 392 ambayo hata hivyo



hayana ubora kwasbabu ni chakavu. Kutokana na uhitaji huo serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha magari mapya yananunuliwa ili kurahisisha shughuli vya ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

# Kulinda rasilimali za maji ni muhimu





Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja akifungua kikao cha Bodi ya Taifa ya Maji, mkoani Morogoro



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja amesema kuendeleza na kutunza rasilimali za maji hapa nchini ni jambo la msingi na lenye faida kubwa kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo kama moja ya urithi katika jamii.

Amesema hayo katika kikao cha Bodi ya Maji ya Taifa mkoani Morogoro na kusisitiza kwa wajumbe wa bodi hiyo kutumia uzoefu wao katika kutoa majibu ya changamoto zinazohusu maji na sio kuegemea katika mabadiliko ya tabianchi kwa sababu miradi ya maji inategemea uwepo wa vyanzo vya maji muda wote

Mhandisi Luhemeja amesema mabadiliko ya hali ya hewa yatumike kubuni mbinu za kuhakikisha maji yanakuwepo nchini, na kuongeza hivi sasa mpango ni kuwa na gridi ya maji nchini, ambayo itaimarisha huduma ya maji katika maeneo yenye upungufu.

Ameitaka Bodi ya Maji ya Taifa kutembelea wadau na kuona changamoto zao ili kupata majibu, kufanya tathmini na kushauri ipasavyo kwa sababu huduma ya maji maana yake ni kuangalia uhai wa Watanzania.

“Tuwe na miundombinu inayotumia maji vizuri na kwa ufanisi” Mhandisi Luhemeja amesema na kuongeza ni vizuri kufanya jambo ambalo kila mwananchi atapata faraja na kuona manufaa yake na kueleza kuwa mwezi Julai 2022 ilizinduliwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Awamu ya Tatu itakayodumu mwaka 2022 hadi 2026 na inahitaji Dola za Marekani bilioni 6.46.

Pia, amesema Wizara ipo katika maandalizi ya Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji ambayo itatekelezwa kuanzia mwaka 2023 hadi 2030 na itagharimu dola za Marekani bilioni 24.7.

Bodi ya Maji ya Taifa inaongozwa na Mwenyekiti Katibu Mkuu mstaafu Mhandisi Mbogo Futakamba.

Tanzania ina maji yanayoweza kupatikana kila mwaka wastani wa mita za ujazo bilioni 126 ambapo mita za ujazo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na mita bilioni 21 ni chini ya ardhi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 na Mabadiliko yake ya Mwaka 2022, Bodi ya Maji ya Taifa ni chombo cha ushauri kwa Waziri wa Maji.

# Ulaya Waipongeza Serikali Ujenzi wa Miradi ya Maji

Mabalozi wa Umoja wa Ulaya (EU) wameridhishwa na ubora wa kasi ya ujenzi wa mradi wa wa maji wa shs bilioni 69 wa Dakio jipya la Maji katika eneo la Butimba Jijini Mwanza.

Mabalozi hao wamepongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Maji kote Nchini za kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

Ujumbe huo wa Mabalozi wa EU umehusisha Waheshimiwa Mabalozi kutoka Umoja wa Ulaya wa nchi za; Ubelgiji, Finland, Ufaransa, Ujerumani, Ireland, Italia, Uholanzi, Hispania na Poland.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Balozi wa EU, Mhe. Manfredo Fanti amesema ujumbe alioambatana nao umeridhishwa na hali waliyoishuhudia ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Butimba.

"Mradi wa Maji wa Butimba ni miongoni mwa miradi inayojengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na baadhi ya Nchi wanachama wa EU; kwa pamoja tumeridhishwa na tumefurahishwa na tuliyoyashuhudia, mradi unakwenda vizuri na ujenzi wake unazingatia ubora, tunaimani utakamilika kwa wakati na hivyo kupunguza adha ya maji kwa wakazi wa Mwanza," Mhe. Balozi Fanti amesema.

Ameongeza ujumbe huo umefurahishwa na jitihada za makusudi za Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwasogezea huduma za kijamii na kuwaletea maendeleo wananchi wake na ameahidi kuwa Umoja wa Ulaya unaendelea kuunga mkono kazi hiyo.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Adam Malima akizungumza na ujumbe huo ofisini kwake, alifikisha salamu za shukrani kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na wananchi wa Mwanza kwa ujumbe huo na sapoti wanayoitoa kwa maendeleo ya wananchi.

"Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba ya wananchi wa Mwanza ninaomba mpokee shukrani zetu za dhati kwa ushirikiano mnaoendelea kutupatia kwa maslahi mapana ya kuimarisha ustawi wa Watanzania



wote," amesema Mhe. Malima.

Aidha, akizungumza wakati wa ziara ya ujumbe huo kwenye mradi wa maji wa Butimba, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Leonard Msenyele amesema amefurahishwa na namna ujumbe huo ulivyoridhishwa na utekelezaji wa mradi.

"Tunajivunia kupokea ugeni huu kwenye miradi yetu hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya miradi ikiwemo huu wa Butimba unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na EU kupitia mkopo wa masharti nafuu," Mhandisi Msenyele amesema.

MD Msenyele amemshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake za kuhahikisha anatafuta fedha za kujenga miradi mbalimbali yenye manufaa kwa wananchi ikiwemo ujenzi wa miradi ya maji.

"Tunamshukuru sana Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kwa namna ambavyo anachukua hatua stahiki za kuhakikisha miradi inatelekezwa kwa wakati na tunamshukuru kwa kutuunganisha na wadau mbalimbali ikiwemo nchi wanachama wa EU ambao wanasaidia kuendeleza miradi," Mhandisi Msenyele amesema.

Mradi wa Maji wa Butimba umefikia asilimia 65 ya utekelezaji na kwamba matarajio ifikapo mwishoni mwa Mwezi Aprili 2023 majaribio ya mradi yataanza na kwamba hadi kufika mwezi Juni 2023 mradi utakuwa umefikisha huduma ya maji kwenye maeneo yaliyokusudiwa.

# Utekelezaji wa mradi wa maji Mugango-Kiabakari umezingatia viwango - Kamati ya Bunge





Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ikitembelea mradi wa maji wa Mugango – Kiabakari – Butiama mapema mwezi Januari 2023. Kamati hiyo imeundwa upya hivi sasa inaitwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira

Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imetembelea mradi wa maji wa Mugango, Kiabakari, Butiama na kuridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo.

Mradi huo unatekelezwa katika chanzo cha maji ya ziwa victoria eneo la Mugango na utagharimu takribani shilingi Bilioni 70.5 ambapo utahudumia zaidi ya vijiji 39 vya Halmashauri za Wilaya ya Butiama na Musoma.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa mradi huo Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Almas Maige (Mb) amesema mradi huo umetekelezwa kwa kuzingatia viwango vya ubora na kuitaka Wizara ihakikishe inasimamia ili ukamilike haraka.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hasan kwa kuonesha nia ya dhati ya kuondoa adha ya huduma ya maji kwa watanzania.

Amesema Wizara itahakikisha inasimamia ili kuhakikisha dhamira ya njema ya Rais ya kumtua mama ndoo kichwani inafanikiwa huku Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Mhe. Sospeter Mhongo akiwataka wananchi wa Musoma Vijijini kuiamini serikali kwani mradi huo utavifikia vijiji vyote vinavyopitiwa na mradi.

Ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira katika Mkoa wa Shinyanga Wilaya Kahama.

Pichani ni Kata ya Tinde, mradi wa maji unaotumia chanzo cha ziwa Victoria na kutoa huduma kwa wananchi, Mradi wa maji wa Tinde-Shelui wenye thamani ya shilingi Bilioni 24.94 . Hatua ya utekelezaji wake ni asilimia 99 na mradi unatarajiwa kuhudumia vijiji takribani 17 vyenye wakazi wasiopungua 87,000









Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa pamoja na viongozi wengine katika ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso amewataka wakandarasi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe kukamilisha kazi zilizosalia katika mradi huo ndani ya miezi 14 kuanzia Machi 2023.

Ametamka hayo wilayani Mwanga wakati wa kusaini makubaliano ya kuhuisha mkataba kati ya Wizara ya Maji na mkandarasi kampuni ya M.A. Kharif & Sons kuhusu kukamilisha ujenzi wa mradi huo.

"Baada ya dhiki ni faraja, na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha za kutosha kumaliza kazi hii" Mhe. Aweso amesema na kusisitiza mkandarasi asiweke sababu zozote za kukwama mradi

Amesema wananchi wamesubiri sana maji, sasa ndani ya miezi 14 lazima wapate majisafi, salama na toshelevu.

Amesema viongozi wa Wizara watafanya kazi usiku na mchana, na kumwelekeza mkandarasi kuweka ratiba ya mpango kazi hadi kukamilisha mradi.

Akiongea kuhusu kazi zilizobaki, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba amesema ni pamoja na kazi ya ulazaji mabomba ambayo yameshafika na kazi inaendelea.

Amesema pia, kuweka mfumo wa umeme ili kusukuma maji kwenda katika matanki, ambapo mradi una idadi ya matanki saba ya kuhudumia wananchi. Hafla hiyo, pamoja na viongozi wengine, imehudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu ambaye amewataka wananchi kushiriki katika miradi ya maji kwa kulinda vyanzo vya maji.



# Mkopo nafuu kuimarisha Mamlaka za Maji – Mha. Luhemeja

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja amezitaka mamlaka za maji nchini kuweka malengo ya makusanyo ili kuona thamani ya kuongeza mtandao wa huduma na idadi ya wateja kupitia mkopo nafuu.

Mhandisi Luhemeja amesema hayo jijini Dar es salaam wakati wa kikao cha kujenga uelewa kuhusu utaratibu uliowekwa kwa mamlaka za maji kuomba mikopo nafuu ya utekelezaji wa miradi ya maji kupitia dirisha la Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF).

"Huu mfuko lazima uangalie namna ya kuisaidia sekta ya maji kuimarika zaidi, na kwa hili nawapongeza sana kwa sababu kila mamlaka ya maji itakuwa na wasaa wa kujiimarisha zaidi kupitia mkopo" Mhandisi Luhemeja amesema na kuongeza kuwa kila mamlaka lazima ipambane kuongeza matokeo ya kazi na kuweka malengo ya makusanyo.

Ameongeza kuwa dirisha la mikopo ni sehemu ya kuongeza mapato katika mamlaka za maji na hatua hiyo itazifanya mamlaka zijipange kukua na kujitegemea.

Mhandisi Luhemeja amesisitiza mikopo irudishwe kuendana na makubaliano yaliyowekwa na sio vinginevyo ambapo riba yake ni asilimia sita.

Ameongeza upo umuhimu wa kukitumia Chuo cha Maji ambacho ni sehemu ya wizara katika kazi mbalimbali za sekta ya maji ikiwamo mafunzo ili kukipa thamani zaidi, pia utunzaji wa rasilimaliza maji ili kuepuka uharibifu na uhaba wa huduma za maji.

Mhandisi Luhemeja ameainisha kuwa mwendo na malengo kwa kila eneo ni upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi kufika asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini, hivyo kila mamlaka ijipime hadi sasa ilipofika.

Moja ya majukumu ya Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) ni kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kusaidia uwekezaji kwenye miradi ya majisafi na miradi ya utunzaji wa vyanzo vya maji, na utoaji wa mikopo utaongozwa na Mwongozo wa Mfuko wa Utoaji Mikopo wa Mwaka 2022.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja



Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Maji Haji Nandule

# Mradi wa Unyambwa Singida wazinduliwa

Katika kuelekea Siku ya Maji Duniani Tarehe 22 Machi Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Peter Serukamba amezindua Mradi wa majisafi wa Unyambwa uliofanikishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA)

Mradi huo umegharimu Tshs milioni 622 ambapo Mkuu wa Mkoa Mhe. Serukamba ameipongeza SUWASA kwa kazi hiyo na mipango mizuri iliyopo ya kuboresha huduma ya maji ili kukabili ongezeko la mahitaji ya maji katika Manispaa ya Singida kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

Amewataka wakazi wa Singida kulipia huduma ya maji, kutunza vyanzo vya maji na miundombinu ya miradi ya maji, kuacha tabia ya wizi wa maji na kufuata taratibu za maunganisho ya maji hatua ambazo zitaipunguzia SUWASA gharama za uendeshaji na kuhudumia wananchi wengi zaidi.

Katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SUWASA amemshukuru Mhe. Serukamba kwa kushirikiana na SUWASA katika kazi mbalimbali na kuahidi kuongeza jitihada ili kufikia lengo la Serikali la kufikisha huduma ya maji mijini kwa asilimia 95 na vijijini asilimia 85 ifikapo 2025.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA Ndugu Sebastian Warioba akieleza kuhusu mradi huo amesema utanufaisha zaidi ya wakazi 6120.



Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Peter Serukamba akizindua mradi wa maji wa Unywambwa unaonufaisha zaidi ya wananchi 6,120




# Hongera

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa DAWASA Ndugu Nelly Msuya ameshinda tuzo ya Afisa Mawasiliano Bora wa Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2022. Tuzo hiyo imetolewa na Chama cha Maafisa Uhusiano Tanzania (PRST) jijini Dar es salaam.



# "Uwekezaji wa Serikali waongeza kiwango cha upatikanaji majisafi" Waziri Mahundi



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahudi (Mb) amesema Serikali inadhamira thabiti pamoja na washirika wa maendeleo kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni 1,035.23 sawa na Dola za Marekani milioni 442.4 ili kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira hapa nchini.

Mhe. Mahundi amesema hayo akifungua Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Maji ambayo pia ni Siku ya Maji Duniani.

Amefafanua uwekezaji huo uliofanyika kati ya Januari hadi Desemba 2022 umeongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 77 vijijini na asilimia 88 mijini na kusisitiza lengo ni kufikia asilimia 85 vijijini na mijini asilimia 95.

"Tunataka pia kufikia lengo la sita la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wote ifikapo2030" Mhe. Mahundi amesema na kuongeza kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali za maji zinazokadiriwa kufika mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka, zinazojumuisha mita za ujazo bilioni 105 juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 chini ya ardhi.

Ameongeza kuwa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi , Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa madogo na ya kati katika Bodi zote za maji za mabonde tisa.

Hatua nyingine, ameainisha ni pamoja na Serikali kutoa fedha za kuendeleza visima vilivyochimbwa katika maeneo ya Kimbiji na Mpera na kutumika kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji katika jiji la Dar es salaam na mkoa wa Pwani. Pia, ujenziwa bwawa la Kidunda umeanza ili kuhakikisha upatikanaji wa majiendelevu jijini Dar es salaam.

Mhe. Mahundi amedokeza kuwa Serikali kwa kushirikiana



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akifungua Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Maji ambayo pia ni Siku ya Maji Duniani.



na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeanza maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa ili kuhudumiajiji la Dodoma.

Amesema suala la kuendeleza rasilimali za maji chini ya ardhi Serikali imelipa kipaumbele na kupitia mfuko wa COVID 19 mitambo ya kuchimba visima seti 25 na vifaa vya ujenzi wa mabwawa seti tano vimenunuliwa.

Awali, akiongea kuhusu Siku ya Maji Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Cyprian Luhemeja amesema Wizara ya Maji imejipanga kuwa na mfumo wa mtandao wa maji wa Taifa (Grid) utakaotoa maji katika maeneo yenye maji mengi ili kupeleka katika maeneo yenye upungufu wa maji.

Leo Machi 22 ni Siku ya Maji Duniani ikiwa na Kaulimbiu ya maadhimisho "Kuongeza Kasi ya Mabadiliko katika Sekta ya Maji kwa Maendeleo Endelevu ya Uchumi"

# HUDUMA YA MAJI YAIMARIKA, MIJINI NA VIJIJINI




Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa maji wa Kigamboni. Kwa nyuma inayoonekana ni taswira ya mitambo ya kisasa iliyonunuliwa na serikali na kusambazwa nchi nzima kwa kila mkoa kwa kazi za Sekta ya Maji, ikihusisha sehemu ya seti 25 za mitambo ya kuchimba visima, seti tano za mitambo uchimbaji na ujenzi wa mabwawa na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi.

Kazi ya huduma ya maji kwa jamii ni baraka. Serikali katika kipindi cha miaka miwili imeimarisha huduma hiyo kwa Watanzania. Hatua hii inasaidia katika kusukuma mbele zaidi kazi na huduma nyingine za maendeleo ambapo huduma ya maji imekuwa chachu kubwa katika kuongeza thamani ya bidhaa mbalimbali.

Ni wazi kuwa maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya binadamu, maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, rasilimali za maji ni kichocheo muhimu katika shughuli za majumbani, kilimo cha umwagiliaji, mazingira, umeme wa nguvu za maji, viwanda, uvuvi, mifugo, madini na utalii. Upatikanaji wa maji kwa ajili ya sekta mbalimbali pamoja na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji ni msingi wa shughuli zote za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa usalama wa Taifa.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea na mwandishi wa makala hii hivi karibuni amesema katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya awamu ya sita, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama vijijini na mijini umezidi kuimarika.

“ Vijijini upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2021 hadi asilimia 77 mwezi Februari 2023. Pia. upatikanaji wa huduma ya maji kwa upande wa mijini umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Februari 2023” Mhe. Aweso amesema.

Ameongeza kuwa hatua hiyo ni azma ya Serikali ya Awamu ya sita katika kuwapatia wananchi majisafi, salama na yenye kutosheleza, pia nia madhubuti ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.

Kazi mbalimbali zimefanyika katika sekta ya maji kwa ushirikiano kati ya viongozi, wananchi na wataalamu wa sekta ya maji.

Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kutekelezwa kwa jumla ya miradi 218 ya mijini na vijijini yenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao milioni 2.09 kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.
“Sanjari na hilo kukamilika kwa jumla ya miradi 1,197 ya usambazaji maji na kutoa huduma kwa wananchi waishio katika vijiji 2,056 nchini ambapo jumla ya Shilingi 401,544,508, 623.00 zimetumika kugharamia miradi hiyo” Mhe. Aweso amesema na kuongeza kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kunafikisha jumla ya vijiji 9,144 vyenye huduma maji nchini. Pamoja na hilo, miradi 150 imeanza kutoa huduma kati ya miradi 177 il-

iyokuwa na changamoto ya utoaji huduma kwa muda mrefu kwa wananchi (miradi chechefu).

Utekelezaji wa programu ya Malipo kwa Matokeo (maarufu kama PforR) umefanyika kwa ufanisi na kuwezesha kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini kutoka Dola za Marekani milioni 350 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 650.

Kuhusu ubora wa maji Tanzania hivi sasa inazo maabara zenye Ithibati na zinaweza kufanya kazi mahali popote hapa Duniani. Maabara za ubora wa maji nchini zenye Ithibati nchini zimeongezeka kutoka moja (Mwanza) mwaka 2021 hadi 7 za Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam; Pia mtandao wa maabara za ubora wa maji nchini umeongezeka kutoka 16 mwaka 2021 hadi kufikia 17 mwezi Februari 2023 kutokana na kuanzishwa kwa maabara ya ubora wa maji ya mkoa wa Manyara.



Mhe. Aweso amesema kiu imejibiwa ya kuona miradi iliyosubiriwa kwa muda mrefu na wananchi ambapo Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka miwili imeanza utekelezaji. Mosi akitaja kusainiwa mikataba na kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 iliyokwama kwa muda mrefu na inaendelea na utekelezaji; pili kusainiwa kwa mkataba na kuanza ujenzi wa bwawa la Kidunda litakalokuwa suluhisho la upungufu wa maji katika mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji katika mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani.

Jambo la tatu kuhusu ujenzi ni kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa ambalo ni tegemeo la utatuzi wa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma na miji ya Bahi, Chemba na Chamwino ambapo hadi mwezi Februari 2023 fidia kwa wananchi wanaopisha mradi imetolewa na taratibu za manunuzi kwa ujenzi zimeanza.





Mhe.Aweso anasema vifaa vya kisasa vya kutoa huduma katika Sekta ya Maji vimenunuliwa ili Watanzania wapate huduma ya maji ya uhakika wakati wote. Amesema vifaa hivyo vimenunuliwa na kuanza kutumika ikiwamo seti 25 za mitambo ya kuchimba visima, seti tano za mitambo uchimbaji na ujenzi wa mabwawa na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi.

Miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Sekta ya Maji jitihada kubwa imefanyika kwa kutekeleza kazi mbalimbali, ili kuwahudumia wananchi, zilizotajwa ni baadhi kati ya kazi nyingi.

Lengo la Serikali hususan katika Sekta ya Maji ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi waishio vijijini unafikia zaidi ya asilimia 85 na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini. Ni wazi kwa mipango iliyopo na kazi zinazoendelea mambo mazuri zaidi kwa wananchi bado yanakuja ilikuimarisha huduma ya maji katika jamii.



**Kitengo cha Mawasiliano**
**ps@maji.go.tz**
Tovuti: www.maji.go.tz